# COVID-19: Mwongozo wa Mpango wa WASH wa kukabiliana na mzuko

**Utangulizi:** Muhtasari wa maelezo muhimu zaidi kuhusu WASH na mzuko wa COVID-19 unaweza kuwa kama ifuatavyo:

- Kunawa mikono mara kwa mara ni hatua muhimu sana ya kuzuia virusi vya COVID-19 kuenea.
- Sehemu za kunawia mikono zinapaswa kupatikana kwa kila mtu ili kuhakikisha kuwa watu wananawa mikono mara kwa mara.
- Lazima kuwe na upatikanaji wa maji safi na ya kutegemewa. Upatikanaji wa visafisha mikono vyenye kemikali za kileo za kuua viini vitasaidia kukomesha virusi vya COVID-19 kuenea.

## Muhtasari wa shughuli za ushughulikiaji za WASH

- Msisitizo wa kunawa mikono na sabuni;
- Ujumbe mfupi wa SMS na / au ujumbe wa redio wa vyombo vya habari;
- Wezesha shughuli za kunawa mikono kupitia vikundi vya waliokamilisha shule na maeneo ya kujivinjari, ili kuwashirikisha vijana kueneza habari na ufuatiliaji baadaye;
- Kutoa ugavi wa ziada wa maji katika Tearfund / Jamii ya wanufaika ambapo idadi ya sasa hairuhusu mahitaji mengine ya kunawa mikono;
- Kuweka klorini katika vyanzo vyote vya mradi wa jamii ili kufikia mkusanyiko wa Ukolevu wa Klorini wa 0.5ppm (au kukubali kuweka klorini nyumbani);
- Kuhamasisha kuhusu hitaji la kusafisha vifaa vilivyopo vya usafi (na kutoa NFI kupitia vocha za pesa taslimu);
- Kuhusisha viongozi wa kidini kutoa ujumbe wazi na thabiti na kushughulikia unyanyapaa na migogoro ndani ya jamii.

## Mkakati

Tearfund na Washirika wa mipango ya WASH **wanapaswa kuunga mkono mamlaka ya afya** ili kushughulikia mzuko:

1. **Kwa nini ni muhimu kudumisha usafi na kunawa mikono;**
2. Upatikanaji wa maji safi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani;
3. Ufikiaji wa mazingira safi kwa vikundi vyote (Vifaa vya Nyumbani na Mbali na Nyumbani), na kusisitiza kuua vijidudu na kusafisha vyoo mara kwa mara vinavyotumiwa na watu ambao wanaonyesha dalili za virusi vya korona;
4. Kushirikiana na huduma za afya ili kuzuia zisiwe vyanzo vya maambukizo ya virusi;
5. Kufanya kazi na viongozi wa makanisa na viongozi wa dini kwa ujumla ili kukuza uhamasishaji wa virusi hivyo, kuhamasisha kukubali mazoea salama ya usafi, na kushughulikia unyanyapaa kwa wanajamii ambao wanaambukizwa / kuonyesha dalili.

Mkakati huu unaweza kutumika katika mipango **yote** ya sasa ya Tearfund / Mipango ya washirika wa Tearfund inayofadhiliwa na WASH. Itakuwa muhimu kutambua vikundi vinavyoweza kudhuriwa ambavyo vinahitaji kupewa kipaumbele katika mkakati huu.

## Sehemu ya 1 - Kwa nini ni muhimu Kudumisha Usafi na Kunawa Mikono

### HWWS - Kunawa mikono kwa sabuni

Tunahitaji kutilia mkazo wa kunawa mikono kwa Sabuni (HWWS). Hatuwezi kupendekeza kufanya mabadiliko ya michakato / njia / zana ambazo tayari zinatumika kukuza HWWS ikiwa matokeo ni mazuri. Hata hivyo, tunahitaji kuweka kipaumbele cha jinsi tunavyowasilisha ujumbe wa kunawa mikono kulingana na mabadiliko ya kijamii na tabia (kv. kubaini mambo ambayo husababisha umati wetu unaolengwa kutumia HWWS).

Kunawa mikono kunapaswa kufanywa kwa **nyakati hizi 5 za muhimu**:

1. Baada ya kutumia choo (**Vifaa vya kunawa mikono vinavyofanya kazi vyenye maji na sabuni vinapaswa kupatikana umbali usiozidi mita 5 kutoka chooni)**;
2. Baada ya kubadilisha nepi ya mtoto;
3. Kabla ya kuandaa chakula;
4. Kabla na baada ya kula:
5. Baada ya kurudi kutoka kazi za mashambani / kushughulikia wanyama.

Kwa sababu ya virusi vya korona, nyakati mbili za ziada za kunawa mikono ni:

6. Baada ya kugusa pua, mdomo, macho au sehemu yoyote ya uso;
7. Baada ya kugusa maeneo yanayoweza kuambukiza.

Ni muhimu kunawa mikono unapoingia mahali pa kazi, shuleni, masoko, sehemu zingine za umma zenye watu wengi, mahali pa kuabudu, na unaporudi nyumbani kwako. Lazima pia mikono ioshwe baada ya kusafiri na treni, mabasi, na teksi, nk.

Kuhusu mbinu za mabadiliko ya tabia, tunaweza kukubaliana na michakato yoyote ifuatayo kulingana na tukio la virusi kwenye eneo lengwa:

**Ambapo matukio ya COVID-19 yako juu au hayajulikani**
Tumia uchunguzi uliopo (kiwango cha HH na data Msingi), matokeo ambayo yanaonyesha vidokezo muhimu vya kunawa mikono kati ya umati unaolengwa. [Timu ya WASH ya Wasimamizi Wengi inaandaa shughuli za utafiti wa kina, kama vile uchunguzi wa KAP na uchambuzi wa vizuizi. *Hii itafanywa **kulingana na** vitendo vya kuongeza viwango vya WASH kama ilivyoorodheshwa hapa chini.]*

**Ambapo matukio ya COVID-19 yako chini, au virusi vimezuiwa**
Zingatia kutumia zana ya [“Wash’Em”], iliyoundwa na London School of Hygiene and Tropical Medicine (LSHTM). *Wash’Em* hutoa njia za kubuni mipango ya haraka ya usafi. Mchakato huo unategemea zana tano za tathmini ya haraka ili kubaini vidokezo muhimu vya kunawa mikono kwa sabuni mara kwa mara. Data iliyokamilishwa imeongezwa kwenye kifaa cha uchambuzi ambacho kitaonyesha vigezo vya kubuni kwa ajili ya mradi wa kunawa mikono.

Wafanyakazi wa Wash'Em katika LSHTM wameshauri kwamba, kwa sababu ya njia ambayo virusi vya korona vinaenea na kuambukizwa kwa urahisi, shughuli za tathmini za haraka zinaweza kuwa hazifai kwa vikundi vyenye washiriki zaidi ya 6, kwa sababu shughuli hizo zinahitaji watu kutangamana. Kwa hivyo tunashauri kwamba mazoea haya ya tathmini ya haraka yanapaswa kutumika tu katika maeneo ambayo matukio ya virusi hivyo viko chini sana, na mahali ambapo kuna hatari ya chini ya kuambukizwa.


Handwashing with soap – our best defence against coronavirus (Kunawa mikono kwa sabuni – kinga yetu bora dhidi ya virusi vya korona) karatasi ya maelezo kutoka kwa zana ya Wash‘Em inajumuisha maoni muhimu ya kuboresha njia za kunawa mikono ***na inapaswa kusomwa na timu zote zinazotekeleza***.

Ingawa vizuizi vimewekwa, shule za Tearfund / zinazofadhiliwa na washirika zitafungwa, na wanafunzi wengi wanaweza kuwa hawaendi shuleni, labda kwa sababu kupunguza hatari ya kuambukizwa, au kumtunza mwanafamilia ambaye ni mgonjwa. Maelezo haya yanaweza kushirikishwa na watoto wakubwa na vijana, ambao wanaweza kuhudhuria vikundi vya nje vya shule au miradi mingine ya kuhamasisha.

## Sehemu ya 2: Upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya nyumbani

### Tippy Tap

Kwa kuwa ni muhimu kunawa mikono, na lazima maji yatumike kwa uangalifu, tunashauri sana kujenga vituo vya kunawa mikono vya gharama nafuu, vinavyohifadhi maji, kama vile “Tippy-Tap”.




Hadi wakati ambapo vocha za NFI zinapatikana, Tippy-Tap ni suluhisho muhimu la muda mfupi.

## Kutia Maji Dawa

Njia za kutia maji dawa ambazo hutumia kuchuja na kuua viini, kama vile kwenye mifumo mingi ya umma ya maji ya kunywa, inapaswa kuua virusi vinavyosababisha COVID-19. Tunapendekeza kutia klorini katika miradi ***yote*** ya maji inayofadhiliwa na Tearfund. Hii inajumuisha miradi ya vyanzo vya maji (kwa mfano, visima na visima vyenye pampu za kutumia mikono, vituo vya ulinzi wa chemchemi ya maji, ambapo watumiaji huteka maji kwenye duka la chanzo kilicholindwa), au kupitia miradi ya usambazaji wa kutumia bomba. Tunapendekeza kudumisha kiwango cha klorini kisichona ukolevu wa (FRC) 0.5ppm, na itatoa karatasi tofauti za mwongozo za kutumia na kuifuatilia. Hii inamaanisha kuwa kwa vyanzo vya maji, klorini inapaswa kuwekwa na wafanyakazi wa kujitolea ambao wamefundishwa kuweka dozi kwenye kisima/chemchemi). Timu za utekelezaji, zinazoshirikiana na mamlaka ya afya na WASH, zinapaswa kuhakikisha kuwa vyanzo vya maji vinapimwa FRC mara kwa mara. Lazima majaribio yafanywe kila siku katika HH.

**Maji ya kunawa mikono:**

**Ujumbe wazi unapaswa kutolewa kwa visambazaji vya maji ambavyo vimelengwa kusambaza maji ya kunawa mikono.** Hii itajumuisha maji ya HH chini ya kiwango cha chini kilichokubaliwa cha 15 lcd [SPHERE]. Sehemu salama za uhifadhi wa maji, kama vile tangi zilizotengenezwa awali au za "kubebeka" zinapaswa kutumika mahali ambapo maji yaliyo ardhini yamehifadhiwa, kutiwa dawa na viini vya maradhi kuuliwa. Tangi ya kuhifadhi maji inaweza kutumika ambapo maji safi yamehifadhiwa.

Kiwango cha maji yanayotumika kunawa mikono kinapaswa kukubaliwa katika kiwango cha mitaa na serikali ya WASH / Mamlaka ya Afya.

**Ufuatiliaji**

Wafanyakazi, iwe wanalipwa au wamejitolea, wanapaswa kupewa uwezo wa kufuatilia huduma ya HH ya usambazaji wa maji katika jamii yao inapohitajika. Tathmini zinapaswa kuzingatia:

- Mahitaji ya usambazaji wa maji kulingana na HH;
- Vituo vya kunawa mikono kuwepo na kutumika (na sabuni)

Ikiwezekana, programu za simu ya mkononi kama Akvo zinapaswa kutumiwa kurekodi uchunguzi. Ikiwa haiwezekani kutumia programu ya simu ya mkononi, karatasi rahisi ya kuweka alama inapaswa kutumiwa.

**Kushirikiana na wanaofaidika**

Tunakusudia kufanya kazi na sehemu ya jamii ambayo inajumuisha wafanyakazi wa kujitolea na wafanyakazi wa Udhibiti wa Maji katika maeneo yanayowezesha:

- Kukuza uhamasishaji wa hatari ya maambukizo ya virusi vya korona ikiwemo
  - kinga
  - dalili, na hatua iliyokubaliwa na wale wanaoambukizwa na virusi
  - sasisho za idadi ya matukio
  - ushauri kwa wahudumu;
- Taarifa ya
  - uchunguzi wa ukadiriaji na vikao vya jamii
  - matokeo ya kampeni ya Wash'Em ya ujumbe wa usafi;
- Arifa ya sera ya nchini na mabadiliko kuhusu
  - upatikanaji wa vituo vya afya
  - shule

- masoko
- makanisa na vituo vya imani
- mahali pa Kazi.

Wanaojitolea wanapaswa kushirikiana kwa karibu na wafanyakazi wa Kituo cha Afya na Wafanyakazi wa Tearfund / Washirika. Mawasiliano na washikadau itakuwa kupitia ujumbe wa maandishi. Mafunzo muhimu na vipindi vya maonyesho yanahitaji kufanywa katika vikao vidogo.

**1. Ufikiaji wa mazingira safi kwa vikundi vyote (Vifaa vya Nyumbani na Mbali na Nyumbani) ni muhimu kuua viini na kusafisha vyoo mara kwa mara vinavyotumiwa na watu ambao wanaonyesha dalili za virusi vya korona;**

Hakuna ushahidi dhabiti kwamba virusi vya COVID-19 vipo kwenye kinyesi cha mwanadamu. Hata hivyo, virusi vinaweza kusambazwa kutoka kwa viini au vimelea katika kinyesi. Matone ya kupumua ni sababu kuu inayojulikana ya ugonjwa huo kuenea. Virusi hivyo huenea kupitia maambukizo ya maeneo na utangamano wa karibu; haswa wakati unatangamana na mtu ambaye ana virusi bila kujua, au anaonyesha dalili.

Ushauri wa WHO uliotolewa katika “Water, sanitation, hygiene and waste management for the COVID-19 virus” (Technical brief, 3rd March 2020) unapendekeza kutumia vyoo tofauti kwa watu ambao wameambukizwa virusi vya COVID-19. Ikiwa haiwezekani kuweka vyoo tofauti, choo kinapaswa kusafishwa na kuua viini vya maradhi mara mbili kwa siku na msafishaji aliyefunzwa ambaye amevaa Vifaa vya Kujikinga vya Kibinafsi (PPE) ambavyo ni gauni, glavu, buti, barakoa, na vitu vya kujifunika usoni au miwani.

Kwa hivyo, ni muhimu sana kwa vyoo kusafishwa mara kwa mara (nyumbani na katika Vituo vya Afya); hasa wakati choo kinashirikishwa na watu wenye dalili za virusi vya korona. Kusafisha vyoo mara kwa mara kutapunguza hitaji la watu kutaka kuwa na choo chao wenyewe ambao wanaonyesha dalili za kuwa na COVID-19. Hii inaweza kufanya matumizi ya maji yanayoweza kutumika tena (mfano maji ambayo tayari yametumika kuoga (WATU AMBAO HAWANA DALILI), au yaliyotumika kusafisha mboga).

Ikiwa vyoo vya ziada vinahitajika katika vituo vya afya, na kuna kiwango cha juu cha maji ya juu ardhini au ukosefu wa nafasi ya kuchimba mashimo ya vyoo, WHO inashauri kwamba takamwili ziwekwe kwenye vyombo vya kuhifadhia maji visivyopenyeza maji na ziachwe kwa muda mrefu iwezekanavyo ili kupunguza viwango vya virusi vinavyowezekana kabla ya kuziondoa kwenye sehemu tofauti kwa ajili ya matibabu ya ziada, utupaji salama, au zote mbili. Mfumo wa tangi mbili unaweza kusaidia kuongeza nyakati za kuhifadhi. Tangi moja inaweza kutumika hadi itakapojaa, kisha kuruhusiwa kutulia wakati tangi ya pili inajaa. Watu wanapasw akuwa makini ili kuzuia kuruka kwa maji na matone wakati wa kusafisha au kuondoa maji ndani ya matangi.

Vitu vifuatavyo Visivyo vya Chakula (NFI) vinapaswa kupatikana kwa kila wanufaika, shule za mradi na vituo vya afya ambavyo tunashirikiana nao. Uangalifu unapaswa kuzingatiwa kwa sababu idadi kubwa inayotolewa na NGO itakuwa na athari hasi katika masoko. Kwa hivyo, tunahimiza ununuzi wa vitu kwenye masoko ya eneo lako inapowezekana. Wauzaji wa mtaa wanapaswa kuhimizwa kukubali uhamisho wa fedha kwa vocha na kutoa vitu vinavyohitajika. Wauzaji wanaweza kulipwa kwa njia kielektroniki bila hitaji la usambazaji wa pesa taslimu. Vitu ambavyo HH itahitaji ni:

- Dawa ya kuondoa madoa

- Vidonge au matone ya Dawa ya Klorini ya Maji (lazima maji yachemshwe ikiwa dawa hii ya maji haipatikani)
- Brashi ya kusugua maeneo
- Ndoo
- Ufagio
- Kemikali za kusafisha
- Jeli yenye kileo zaidi ya asilimia 60%
- Sabuni ya kunawa mikono
- Sabuni ya kufulia kwa mashine na kufua kwa mikono

**2. Kushirikiana na huduma za afya ili kuwazuia kuwa vyanzo vya maambukizo ya virusi**

Katika nchi nyingi, ambapo matukio ya kwanza ya COVID-19 yameripotiwa, serikali inadhibiti kikamili hali hiyo. Mtu atapimwa ikiwa anatuhumiwa kuwa na virusi vya COVID-19 na Ikiwa matokeo yanaonyesha ana Covid -19, mtu huyo atatengwa na kutibiwa. Hii inafuatwa na utafutaji wa watu waliotangamana, kupima watu waliotangamana nao na pia kuua viini katika jengo hilo.

Ni muhimu kwa Tearfund na washirika wao kuchukua jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba maelezo sahihi kuhusu COVID-19 na jinsi ya kuzuia kueneza zaidi inachapishwa kadri iwezekanavyo. Wagonjwa ambao wamepata nafuu kutoka kwa virusi wanaweza kuwa bora kufanya hivyo.

*Lazima za wafanyakazi ambazo zinashirikishwa na waathirika na wanajamii wengine wanaohusika katika kupunguza maambukizo ya virusi zichunguzwe na kuthibitishwa na wafanyakazi wetu wa WASH na shirika husika la serikali la WASH / Afya. Hii ni kuhakikisha kuwa ujumbe na mapendekezo ambayo yanashirikishwa yanaunga mkono mazoea mazuri.*

Kila nchi iko katika awamu tofauti ya virusi vya COVID-19. Kwa hivyo, njia za kutuma ujumbe zitakuwa tofauti.Ziara za nyumba hadi nyumba na mikutano ya jamii ni njia moja ya kuhakikisha maelezo yamewasilishwa, ***ikiwa tu ni salama kufanya hivyo***.

Tunaandaa njia salama za kutekeleza ziara za HH wakati wa mzuko huu wa Virusi vya Korona. Ni muhimu kuendelea na majukumu na ushauri wa sasa kuhusu kujitenga na watu:

- kutoingia nyumbani
- kudumisha umbali wa mita 2 na kila mtu
- kutosalimiana kwa mikono
- salamu nyingine za kugusana kimwili
- n.k.

Hata hivyo, mara tu nchi ikithibitisha kwamba kuna visa vya Virusi vya Korona, basi mikutano na mikusanyiko inapaswa kukomeshwa na kuepukwa kama ilivyoelekezwa na serikali.

Timu za mradi wa nchi wa WASH ina ushirikiano thabiti na wizara ya Maji. Hata hivyo, huenda kukosa kuwa na mahusiano thabiti na wizara ya Afya. Maeneo muhimu ambayo yatasaidia Tearfund na washirika wake kushirikiana vyema na huduma Afya ni:

1. Kutambua kuwa ni jukumu la serikali kulinda raia wake. Kwa kawaida, Wizara ya Afya katika nchi binafsi, yenye usaidizi kutoka WHO, ambao watatoa ushauri kuhusu ushughulikiaji wa changamoto.

2. Tearfund na washirika wanapaswa kushirikiana na mamlaka husika ya afya. Hii inaweza kuwa katika kiwango cha kitaifa, mkoa au mitaa kulingana na uhusiano wa sasa na upatikanaji wa mradi. Njia rahisi itakuwa kutumia wawakilishi wa Wizara ya Maji ambao miradi ya WASH hufanya kazi nao. Viongozi wa jamii pia wanaweza kuwasiliana na wawakilishi wa Wizara ya Afya.

3. Kutambua mipango na ujumbe wa kipaumbele ambao Wizara ya Afya inayo. Hata hivyo, pia unapaswa kuwa tayari kusikiliza na 'kushawishi kimya kimya' ujumbe wa kipaumbele endapo kuna utofauti mkubwa ambao unaweza kuhitaji kusahihishwa. Ni wakati huu tunapaswa kuonyesha jinsi tunavyoweza kuongeza thamani na kuunga mkono ushughulikiaji huu.

4. Kuwa tayari kujaza mapengo. Mipango itafanywa vizuri lakini fedha zitahitajika ili kuianzisha k.m. ununuzi wa sabuni, kisafisha mikono chenye kemikali za kileo za kuua viini, malipo kwa wafanyakazi wa jamii wa huduma ya afya, malipo ya uhamasishaji wa watu wengi (*k.m. maonyesho* ya redio) nk.

## Sehemu ya 3: Kushirikiana na Viongozi wa Kanisa ili Kukuza Uhamasishaji, Mazoea Salama ya Usafi na Kushughulikia Unyanyapaa ndani ya jamii.

Watu hawanawi mikono kwa sababu ni vigumu au kwa sababu wameweka vipaumbele vingine. Kwa hivyo, ili kubadilisha tabia ya kunawa mikono tunahitaji kuunda mazingira ambapo ni rahisi kufikia vituo vya kunawa mikono. Kwa kufanya hivi itanya kuna mikono kitu cha kupendeza kufanya. Katika milipuko, kawaida watu huanza kunawa mikono yao mara kwa mara na vizuri zaidi. Hii ni kwa sababu wanajiona kuwa wanaweza kupata magonjwa kuliko kawaida. Tunapaswa kuunga mkono na kuhimiza badiliko hili katika tabia bila kuleta uwoga usiohitajika na kufanya hivyo kwa njia ambayo inafanya kunawa mikono kuwa tabia ambayo itaendelea hata baada ya mlipuko huu.

Ni muhimu kwa viongozi wa dini zote kusaidia kutuma ujumbe sahihi na kuonyesha kuunga mkono jamii. Pia ni muhimu kwa viongozi wa dini kushughulikia kwa usahihi hali za unyanyapaa au za uhasama zinazoonyeshwa watu ambapo inaaminika wanaweza kuleta hatari zaidi kwa eneo hilo, kuonyesha dalili za virusi vya COVID-19. Haichukuliwi kwamba kiongozi wa imani ana uwezo huu na kwa hivyo mafunzo kuhusu kutuma ujumbe na kufikia jamii ni sehemu muhimu ya mkakati wa mawasiliano wa COVID-19. Ilimradi iwe salama kufanya hivyo tunapendekeza kwamba viongozi wa imani na dini zote wakutane mara kwa mara ili kukubaliana kuhusu ujumbe wanaotuma. Ni muhimu kwamba kila mmoja apokee ujumbe huo mmoja ambao una mipasho sahihi ya maelezo na ushauri.
Tafadhali rejelea Mitigating COVID19 for church groups and religious gatherings (Kupunguza hatari ya COVID-19 kwa vikundi vya makanisa na mikusanyiko ya kidini) kwa mwongozo wa ziada wa kujihusisha na viongozi wa kanisa na wa imani.

## Ulinzi wa wafanyakazi wa Tearfund na wafanyakazi wenza wanaohusika na utekelezaji wa WASH

### Usafi wa kibinafsi:

1. Kunawa mikono kwa sabuni mara kwa mara;

2. Hewa safi ya kupumua - Unapokohoa na kupiga chafya, funika mdomo na tishu au kiwiko kilichokunjwa, weka tishu ndani ya pipa iliyofungwa na unawe mikono;

3. Kugusa uso – Epuka kugusa macho, pua au mdomo wako.

**1. Kunawa mikono kwa sabuni (usafi wa mkono**)

- Kunawa mikono wa mara kwa mara na sahihi ndiyo ***njia moja bora*** ambayo inaweza kutumika kuzuia kuenea kwa virusi vya COVID-19.
- Mikono inapaswa kusafishwa kwa sabuni na maji kwa sekunde 20–30 kwa kutumia mbinu inayofaa:



2. **Visafisha mikono (usafi wa mkono)** – Ikiwa hakuna uchafu unaoonekana kwenye mikono, kisafisha mikono chenye kemikali za kileo za kuua viini kinaweza kutumika kwa sekunde 20–30 kwa kutumia mbinu inayofaa.



tearfund

## Usafi katika Maeneo ya Umma/Ofisini:

1. **Kujitenga na jamii** – Kaa umbali wa angalau mita 2 (futi 6) kati yako na watu wengine, haswa wale wanaokohoa, kupiga chafya na wenye homa.
2. **Mkusanyiko wa watu** – Epuka umati. Matukio yenye watu wengi yanapaswa kupigwa marufuku ili kukomesha kuenea kwa virusi vya COVID-19.
3. **Kutupa uchafu** – Ni muhimu kuwa na mapipa ya matumizi yenye vifuniko vilivyowekwa katika maeneo ya pamoja, ya kutupa tishu.
4. **Safisha maeneo mara kwa mara** – Maeneo ya pamoja yanapaswa kusafishwa mara kwa mara, hasa bafu inapaswa kusafishwa kila siku. Ikiwa bidhaa za matumizi za kuua viini hazipatikani kwa urahisi, dawa ya kuua viini inaweza kutengenezwa kutoka kwa dawa ya kuondoa madoa ya matumizi ya nyumbani (yenye asilimia 5 ya hipokloridi ya sodiamu). Tumia uwiano wa kipimo 1 cha dawa ya kuondoa madoa ya matumizi ya nyumbani kwa vipimo 9 vya maji.
5. **Weka vituo vya kunawia mikono kwa sabuni**, na utambue mtu ambaye anaweza kuwakumbusha wengine kunawa mikono yao, na kufuatilia upatikanaji wa sabuni, maji na tishu kwenye vituo hivyo. Anapaswa pia kuwakumbusha watu kunawa mikono yao mara kwa mara. Vituo vyenye kisafisha mikono vinapaswa kupatikana na lazima vitumiwe wakati wowote wafanyakazi wanaingia ofisini.

---

## RASILIMALI:

**Tovuti kamili ya rasilimali ya WASH ya kufahamisha ushughulikiaji yetu ya COVID-19 imetolewa kwenye:**

Global WASH Cluster COVID-19 Resources

Rasilimali Kuu za COVID-19 za Kishada cha WASH

**Frank Greaves** Kiongozi wa WASH, Frank.greaves@tearfund.org
**Charles Macai** Mshauri wa Roving WASH, anayelenga ECA, Charles.macai@tearfund.org
**Munya Charuka** Mshauri wa Roving WASH, anayelenga SEA/WA, Munyaradzi.charuka@tearfund.org